

﴿إِلَيْهِ يَصْعَدُ الْكَلِمُ الطَّيِّبُ وَالْعَمَلُ الصَّالِحُ يَرْفَعُهُ﴾

سلسلة الكلم الطيب - رقم: ٥

MFULULIZO WA MANENO MAZURI - NAMBA 5

قال محدث الخراسان

عبد الله بن المبارك المروزي:

«في صحيح الحديث شُغِلَ عَنْ سَقِيمِهِ»

[الجامع، للخطيب البغدادي: (٣٣٤/٨)، رقم: (١٤٩١)]

**UBAINFU JUU YA
UDHAIFU WA HADITHI YA
MAKUMI MATATU YA RAMADHANI**

- 1.KUMI LA REHMA**
- 2.KUMI LA MSAMAHA**
- 3.KUMI LA KUACHWA HURU NA MOTO**

Mwandishi

Ismaili Bin Musa Bin Kiza

Neno la mwandishi

سلسلة الكرم الطيب

MFULULIZO WA MANENO MAZURI

Ni mfululizo wa risala na makala za kielimu zenye lengo la kuondoa au kupunguza ujinga wa kutoifahamu dini, katika jamii za waislamu.

Hii ni makala namba 5, naitanguliza kwa waislamu wote wenye uwezo wa kusoma na kuelewa Lugha ya Kiswahili, ikibainisha **Udhaifu wa Hadithi ya Makumi Matatu ya Ramadhani**.

Na nimeigawa katika sehemu mbili

Sehemu ya kwanza: Nimeelezea umuhimu wa Elimu ya Hadithi na nafasi ya Hadithi za Mtume **(Swallal Laahu Alayhi Wasallam)**

Sehemu ya pili: Udhaifu wa Hadithi ya Makumi Matatu ya Ramadhani.

Namwomba Allah **(Sub-hanau Wata-'ala)** ainufaishe makala hii, kama alivyozinufaisha zile zilizotangulia, na anipe Ikh-las katika hii amali tukufu, na anisamehe pale nitakapoteleza, hakika yeye ni mwingi wa huruma na mwisngi wa kusamehe.

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

Mwandishi

Abu Anas

Ismaili Bin Musa Bin Kiza

Markaz Bin Taymiyyah

Pongwe – Tanga - Tanzania

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ، نَحْمَدُهُ وَنَسْتَعِينُهُ وَنَسْتَغْفِرُهُ، وَنَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ شُرُورِ أَنْفُسِنَا، وَمِنْ سَيِّئَاتِ أَعْمَالِنَا، مَنْ يَهْدِهِ اللَّهُ فَلَا مُضِلَّ لَهُ، وَمَنْ يَضِلَّ فَلَا هَادِيَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَشْهَدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ.

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تُقَاتِهِ وَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنْتُمْ مُسْلِمُونَ﴾ [آل عمران: ١٠٢]

﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِنْ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ وَخَلَقَ مِنْهَا زَوْجَهَا وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالًا كَثِيرًا وَنِسَاءً وَاتَّقُوا

اللَّهِ الَّذِي تَسَاءَلُونَ بِهِ ءَالِ الرَّحَامِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَيْكُمْ رَقِيبًا﴾ [النساء: ١]

﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَقُولُوا قَوْلًا سَدِيدًا ﴿٧٠﴾ يُصْلِحْ لَكُمْ أَعْمَالَكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ وَمَنْ يُطِيعِ

اللَّهِ وَرَسُولَهُ فَقَدْ فَازَ فَوْزًا عَظِيمًا ﴿٧١﴾﴾ [الأحزاب: ٧٠ - ٧١]

أَمَّا بَعْدُ: فَإِنَّ أَصْدَقَ الْحَدِيثِ كِتَابُ اللَّهِ، وَخَيْرَ الْهَدْيِ هَدْيُ مُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ، وَشَرُّ الْأُمُورِ مُخَدَّثَاتُهَا، وَكُلُّ مُخَدَّثَةٍ بَدْعَةٌ، وَكُلُّ بَدْعَةٍ ضَلَالَةٌ، وَكُلُّ ضَلَالَةٍ فِي النَّارِ.

SEHEMU YA KWANZA UMUHIMU WA ELIMU YA HADITHI

Umuhimu wa Elimu ya Hadithi na ubora wake

Hakika Elimu ya Hadithi ni katika elimu zinazomkurubisha mja kwa Mola wake, hilo linatokana na elimu hii kushughulikia maneno na vitendo vya Mbora wa Viumbe, nae ni Mtume Muhammad (Swallal Laahu Alayhi Wasallam).

Katika ubora na umuhimu wa elimu hii ni kule kupambanua kilichosihi na kisichosihi miongoni mwa maneno na vitendo vya Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam), kwani lau si elimu hii kuwepo katika ulimwengu, na juhudi za wanachuoni katika kuisomesha na kuitawanya katika miji mbalimbali, basi sisi waislamu tungemuambudu Allah kwa ujinga, kama wanavyomuambudu Manaswara (Wakristo).

Na watu wenye kujishughulisha na elimu hii ni wachache katika kila zama na kila mahala, bali ipo baadhi ya miji hakuna kabisa elimu hii, kutokana na ugumu na uzito uliopo katika elimu hii, ndio maana akasema Imamu Bukhariy:

[أَفْضَلُ الْمُسْلِمِينَ رَجُلٌ أَحْيَا سُنَّةَ مَنْ سَنَّ الرَّسُولِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَدْ أُمِيتَتْ،

فَاصْبِرُوا يَا أَصْحَابَ السُّنَنِ رَحِمَكُمُ اللَّهُ فَإِنَّكُمْ أَقَلُّ النَّاسِ]

[Aliyembora katika waislamu ni mtu ambae amehuisa sunna miongoni mwa sunna za Mtume (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**) zilizofishwa, basi subirini enyi watu wa suna, Allah awarehemu, hakika nyinyi ni watu wachache mno].

Watu wa Sunna anaowakusudia hapa Imamu Bukhariy ni watu wanaojishughulisha na elimu ya Hadithi, ndio maana baada ya Al-khatwibul Bagh-daadiy kuitaja kauli hii akasema:

[صَدَقَ رَحْمَهُ اللَّهُ فِي قَوْلِهِ، لِأَنَّكَ إِذَا اعْتَبَرْتَ لَمْ تَجِدْ بَلَدًا مِنْ بُلْدَانِ الْإِسْلَامِ يَخْلُو مِنْ فِقْيِهِ، أَوْ مُتَّفَقِهِ يَرْجِعُ أَهْلُ مِصْرِهِ إِلَيْهِ، وَيُعَوَّلُونَ فِي فَتَاوِيهِمْ عَلَيْهِ، وَتَجِدُ الْأَمَّصَارَ الْكَثِيرَةَ خَالِيَةً مِنْ صَاحِبِ حَدِيثٍ، عَارِفٍ بِهِ مُجْتَهِدٍ فِيهِ، وَمَا ذَاكَ إِلَّا لِصُعُوبَةِ عِلْمِهِ، وَعِزَّتِهِ، وَقِلَّةِ مَنْ يَنْجُبُ فِيهِ مِنْ سَامِعِيهِ وَكَتَبْتِهِ]

[Amesema kweli Imamu Bukhari Allah amrehemu katika kauli yake, kwa sababu pindi utakapozingatia hutopata mji wowote miongoni mwa miji ya kiislamu umekosa mwanachuoni wa Fiq-hi, au mtu wa Fiq-hi watu wa mji wake wanarejea kwake, na wanategemea fatawa zao kwake. Na utapata miji mingi imekosa watu wa hadithi, wenye ujuzi na kujitahidi, na halikuwa hilo isipokuwa ni kutokana na ugumu wa elimu yake, na uchache wa wenye kuingia katika elimu hiyo wenye kuisikiliza na kuiandika].

⇒ Tazama kauli hii na ile ya Imamu Bukhari, katika kitabu chake: Al-jaamiu Li-akh-laaqi Raawiy Wa-aadaabis Saami-'i, Jz. 1, Uk. 30, Na. 90.

Amesema kweli Imamu Al-khatwiibul Bagh-daadiy Allah amrehemu, kwani hali ya hapa nchini kwetu ni ushahidi tosha juu ya hili, zaidi ya miaka 50 sasa tokea Tanzania ipate uhuru, haijapata mwanachuoni wa hadithi anayetambulika Afrika Mashariki, achilia mbali duniani.

Nafasi ya hadithi za mtume katika dini

Kila muislamu mwenye kujishughulisha na elimu, bali hata yule wa kawaida anayefuatilia dini yake, anafahamu nafasi ya Hadithi za Mtume wetu Muhammad (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**) katika dini.

Hadithi za Mtume ndio zenye kuifasiri Qur-aan na kubainisha maana na makusudiwa yake, kama alivyosema Allah (**Jalla Jalaaluh**) katika Suratu Nah-li (16), aya ya 44:

﴿وَأَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الذِّكْرَ لِتُبَيِّنَ لِلنَّاسِ مَا نُزِّلَ إِلَيْهِمْ﴾

[Na tumeteremsha kwako wewe –Muhammad– ukumbusho ili ubainishe kwa watu kile ambacho kimeteremshwa kwao]

Kutokana na kazi hii aliyopewa Mtume (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**), Allah (**Sub-haanahu Wata-'ala**) akamlinda na kutamka makosa, akakifanya kinywa chake kitakatifu na kitwahaarifu hakitamki ila haki peke yake, akasema Allah (**Sub-haanahu Wata-'ala**) katika Suratu Naj-mi (53), aya ya: 4 – 5.

﴿وَمَا يَطِقُ عَنِ الْهَوَىٰ ۗ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْيٌ يُوحَىٰ﴾

[Na -Mtume- hatamki kwa matamano ya nafsi yake. Isipokuwa -anatamka kutokana na- Wahyi uliofunuliwa kwake].

Anachokitamka Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) ni kweli na ni haki ambayo haina shaka kwa kila muislamu.

Muislamu hawezi kutekeleza ibada yoyote kwa ukamilifu wake bila ya kutumia hadithi, hawezi kufahamu maana sahihi ya Qur-aani na bila ya kutumia hadithi, hivyo hadithi za Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) zinanafasi kubwa katika dini kama nafasi ya kichwa katika kiwiliwili cha mwanadamu.

Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) kuwa amesema:

[أَلَا إِنِّي أُوتِيتُ الْكِتَابَ وَمِثْلَهُ مَعَهُ، أَلَا إِنِّي أُوتِيتُ الْقُرْآنَ وَمِثْلَهُ مَعَهُ]

[Tambueni!, Hakika mimi nimepewa Kitabu na mfano wake pamoja nacho. Tambueni!, Hakika mimi nimepewa Qur-aani na mfano wake pamoja nayo].

⇒ Hadithi hii ni sahihi, ameisimulia Swahaba Mtukufu Miq-daam Bin Ma-'adii Karib Alkindiy (Allah amridhie), na ameitaja:

1. Imamu Ahmad, katika **Musnadi** yake, Jz. 28, Uk. 410, Hadithi Na. 17174.
2. Imamu Abu Daud, katika **Sunani** yake, Hadithi Na. 4604.

Yaani Mtume amepewa Qur-aan ili ailete kwetu, halafu akapewa kitu kingine pamoja na hiyo Qur-aan, kitu chenyewe **ni kubainisha Qur-aani, na kitu hicho ni Hadithi au Suna zake.**

Juhudi za wanachuoni wa kiislamu katika hadithi

Wanachuoni wa kiislamu kuanzia Maswahaba wa Mtume na wale waliyokuja baada yao hadi katika karne hizi za sasa, kwa hakika wametoa juhudi kubwa sana katika kuhifadhi hadithi za Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam).

Miongoni mwa juhudi hizo ni kuzihifadhi hadithi kwenye vifua vyao, kisha kuziandika kwa udhibiti wa hali ya juu katika vitabu vyao, huku wakihakikisha wanayachunga maneno ya Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) yasichanganyike na maneno ya yeyote katika wao.

Wakaweka misingi na kanuni za kupokea Hadithi, kuandika, kusimulia, namna ya kupokea na namna ya kusimulia, misingi na kanuni ambazo lau mtu yeyote atajaribu kuingiza neno moja katika maneno ya Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) basi atajulikana yeye na kile alichokiingiza.

Ukisoma Elimu ya Mustwalahul Hadiith, au kwa jina lingine: Usuulul Hadiith, au Usuulu Riwaayah, utaiona juhudi hiyo ya ajabu kabisa ambayo haina mfano, haijawahi kutoka katika umma wowote miongo mwa umma zilizotangulia, wala huwezi kuifanisha na juhudi yoyote ile iliyotolewa na wanachuoni wengine katika kulinda fani zao, na kwa faida zaidi ya kujua

juhudi hizi, soma kitabu: **Tad-wiinus Sunnatin Nabawiyyah** cha Dkt. Muhammad Bin Matwar Azzah-raaniy, utafaidika zaidi.

Vitimbi vya maadui wa dini katika hadithi

Pamoja na juhudi hizi kutolewa na wanachuoni wetu katika kila zama, lakini kwa upande wa pili wa maadui wa dini hii tukufu nao hawakulala wala kurudi nyuma, walihakikisha wanaiharibu dini hii kupitia kila upande na njia itakayowezekana kwao hata kama itagharimu maisha yao.

Baada ya maadui hao kufahamu nafasi ya Hadithi za Mtume katika dini, na namna waislamu wanavyoziheshimu, walitoa juhudi kubwa sana kuhakikisha wanaingiza maneno yao, au kupunguza, au kuongeza katika maneno ya Mtume, kwa lengo la kuharibu dini ya uislamu.

Wakajitokeza baadhi ya watu (huko zamani na hadi sasa) wenye lengo baya na dini hii, wakajichomeka katika safu za waislamu, na wengine katika safu za wanachuoni wa kiislamu, wakasoma kwa wanachuoni hao si kwa lengo la kuihifadhi sheria na kuilinda, bali kwa lengo la kuijua sheria ili waweze kuiharibu kwa njia za kielimu.

Wakafanikiwa kutunga hadithi zao kwa kuziingilia hadithi za Mtume (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**), wakapunguza maneno au kuongeza, kisha wakazileta katika jamii kwa sura kana kwamba ni Hadithi za Mtume kumbe ni maneno yao, au maneno ya Mtume lakini wameyapunguza au kuongeza.

Wanachuoni wa kiislamu wakaujua huu mchezo mchafu

Lakini kutokana na misingi iliyowekwa na wanachuoni wa hadithi katika kuyachunga maneno ya Mtume (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**) yasichafuliwe, wala yasiongezwe au kupunguzwa, maadui hawa walijulikana mapema sana, wakabainishwa na kudhibitiwa majina yao katika vitabu maalum ambavyo viliandikwa na wanachuoni wetu, huku wakimbainisha kila mmoja na kile alichokiweka, au kukiongeza au kukipunguza.

Miongoni mwa vitabu vilivyoandikwa kwaajili ya kuwabainisha watu waliokuwa na huu mchezo mchafu wa kutunga hadithi na kuzinasibisha kwa Mtume, au kuzichezea hadithi za Mtume kwa kuongeza au kupunguza maneno ni:

1. **Kitaabu Dhwu-'afaaul Kabiir**, cha Abu Ja-'afar Muhammad Bin Omar Bin Musa Bin Hamaad **Al-'uqayliy** (Kf. 322^H=934^M).
2. **Kitaabul Maj-ruuhiina**, cha Abu Hatim Muhammad Bin Ahmad Bin Hibbaan (Kf. 354^H=965^M)
3. **Al-mugh-niy Fii Dhwu-'afaai**, cha Shamsu Diin, Abu Abdillahi Muhammad Bin Othman **Addhahabiy** (Kf. 748^H=1347^M)

Pia wakaandika vitabu maalum katika kubainisha Hadithi Dhaifu na sababu ya udhaifu wake, miongoni mwa vitabu hivyo ni:

1. Al-maw-dhwuu-'aatul Kubraa, cha Jamaalu Diin Abdurahman Ibnul Jawziy (Kf. 597^H=1201^M)
2. Al-la-aalul Masw-nuu-'ah Fil Ahaadiithil Maw-dhwuu-'ah, cha Jalaalu Diin Abdurahman Bin Abibakri Assuyuutwiyy (Kf. 911^H=1505^M)
3. Sil-silatul Ahaadiithi Dhwa-'iifah Wal-maw-dhwuu-'ah, cha Abu Abdirahman Muhammad Bin Nuuh Bin Haaj Naaswiru Diin Al-baniy (Kf. 1420^H=1999^M)

Allah awarehemu wanachuoni hao, kwani bila ya wao, sisi tusingeweza kufahamu wala kupambanua maneno ya Mtume (**Swallal Laahu Alayhi Wasallam**) na mwingine asiyekuwa Mtume, na tungekuwa kama Manaswara katika kuabudu kwao, kwani wao hawawezi kupambanua maneno ya Mitume na maneno ya watu.

SEHEMU YA PILI **HADITHI YA MAKUMI MATATU**

Baada ya kufahamu umuhimu wa Elimu ya Hadithi, na nafasi ya Hadithi za Mtume katika dini, katika hii sehemu ya pili na ya mwisho tutafahamu **Udhaifu wa Hadithi ya Makumi matatu ya Ramadhani**, hadithi ambayo inatumiwa sana na Masheikh, Walimu, Makhatibu wa Ijumaa na Wahadhiri mbalimbali wa dini, hasa katika kipindi hiki cha Ramadhani, wakiwa na lengo zuri la kuwahamasisha waislamu kwenye kuongeza juhudi ya amali njema, lakini wakimzulia Mtume kwa kumsema asiyoyasema.

Matumizi ya Hadithi dhaifu na za uongo katika mambo ya dini hayakuanza leo wala jana, bali jambo hili lilianza tokea karne ya kwanza baada tu ya Mtume kufariki kwa miaka michache, isipokuwa jambo hili kwa wakati huo lilikuwa ni dogo kulingana na uwepo wa wanachuoni wengi wa kiislamu hasa Maswahaba.

Lakini kila zama zilipozidi kupita na uislamu kuingia katika miji mbalimbali, na wanachuoni kuwa wachache katika miji hiyo, matumizi ya **Hadithi Dhaifu** na za **Uongo** yalizidi, jambo ambalo liliwapelekea wanachuoni wa hadithi pamoja na uchache wao; kuongeza juhudi ya kuwabainisha watungaji wa hadithi hizo pamoja na hadithi zao.

Ama katika hii miji yetu, jambo ni kubwa na hali ni mbaya sana, hasa kutokana na elimu hizi za hadithi kuchelewa kuingia katika miji mingi hapa nchini Tanzania.

Hivyo utawaona viongozi wengi wa dini wakitumia hadithi dhaifu bali nyingine ni za uongo, kiasi ambacho ukimuangalia kiongozi huyo, na namna jamii inavyomsikiliza, haendani kabisa na kutojua udhaifu wa hadithi kama hiyo, lakini kwa kuwa hakujishughulisha na Elimu ya Hadithi, basi kila akizungumza kuhusu hadithi utamuonea huruma namna anavyopoteza mwelekeo kwa kuacha hadithi sahihi na kushikamana na Hadithi Dhaifu na za uongo.

Katika kuifafanua hadithi hii tutatumia hatua mbili:

Hatua ya kwanza: Tutaitaja hadithi yote kama ilivyo katika vitabu vya hadithi, huku tukitegemea tamko lililotajwa na Imamu Bin Khuzayma katika Sahihi yake.

Hatua ya pili: Tutataja hukumu waliyoitoa wanachuoni juu ya hadithi hii na sababu ya kutoa hukumu hiyo.

Hatua ya kwanza: Matini ya Hadithi.

[عَنْ عَلِيِّ بْنِ زَيْدِ بْنِ جُدْعَانَ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ الْمُسَيَّبِ، عَنْ سَلْمَانَ الْفَارِسِيِّ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ، قَالَ: خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ - صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - فِي آخِرِ يَوْمٍ مِنْ شَعْبَانَ، فَقَالَ]

[Kutoka kwa Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan, kutoka kwa Saidi Bin Musayyab, kutoka kwa Salmaan Al-faarisiy (Allah amridhie) amesema: Alituhutubia Mtume wa Allah (Swallah Laahu Alayhi Wasallam) siku ya mwisho katika Mwezi wa Shabani, akasema]

[أَيُّهَا النَّاسُ، قَدْ أَظَلَّكُمْ شَهْرٌ عَظِيمٌ، شَهْرٌ مُبَارَكٌ، شَهْرٌ فِيهِ لَيْلَةٌ خَيْرٌ مِنْ أَلْفِ شَهْرٍ، جَعَلَ اللَّهُ صِيَامَهُ فَرِيضَةً، وَقِيَامَ لَيْلِهِ تَطَوُّعًا، مَنْ تَقَرَّبَ فِيهِ بِخَصْلَةٍ مِنْ الْخَيْرِ، كَانَ كَمَنْ أَدَّى فَرِيضَةً فِيمَا سِوَاهُ، وَمَنْ أَدَّى فِيهِ فَرِيضَةً، كَانَ كَمَنْ أَدَّى سَبْعِينَ فَرِيضَةً فِيمَا سِوَاهُ]

[Enyi watu, hakika umekurubia kuingia kwenu mwezi mtukufu, mwezi wenye baraka, mwezi ambao ndani yake kuna usiku mmoja ni mbora usiku huo kuliko miezi elfu moja isiyokuwa na usiku huo, Allah amejaalia funga yake ni lazima, na kisimamo chake ni suna, atakaejikurubisha kwa Allah ndani ya mwezi huu kwa kufanya jambo lolote la kheri (sunnah), atakuwa ni kama yule ambaye ametekeleza faradhi katika miezi mingine, na atakaetekeleza faradhi ndani yake, atakuwa kama mtu aliyetekeleza faradhi sabini katika miezi mingine usiokuwa huu]

[وَهُوَ شَهْرُ الصَّبْرِ، وَالصَّبْرُ ثَوَابُهُ الْجَنَّةُ، وَشَهْرُ الْمَوَاسَاةِ، وَشَهْرٌ يَزْدَادُ فِيهِ رِزْقُ الْمُؤْمِنِ، مَنْ فَطَّرَ فِيهِ صَائِمًا كَانَ مَغْفِرَةً لِدُنُوبِهِ، وَعَثَقَ رَقَبَتَهُ مِنَ النَّارِ، وَكَانَ لَهُ مِثْلُ أَجْرِهِ مَنْ غَيْرَ أَنْ يَنْتَقِصَ مِنْ أَجْرِهِ شَيْءٌ]

[Nao ni mwezi wa subira, na subira thawabu zake ni pepo, ni mwezi wa kuliwazana, ni mwezi ambao riziki ya muumini inazidi, atakaemfuturisha mwenye kufunga, atakuwa ni mweye kusamehewa madhambi yake, na kuiacha huru shingo yake na moto, na atakuwa na ujira mfano wake pasi na kupunguza chochote katika ujira wake]

[قَالُوا: لَيْسَ كُنَّا نَجِدُ مَا يُفَطِّرُ الصَّائِمَ. فَقَالَ: "يُعْطِي اللَّهُ هَذَا الثَّوَابَ مَنْ فَطَّرَ صَائِمًا عَلَى تَمْرَةٍ، أَوْ شَرْبَةِ مَاءٍ، أَوْ مَذْقَةٍ لَبَنٍ، وَهُوَ شَهْرٌ أَوْلَاهُ رَحْمَةٌ، وَأَوْسَطُهُ مَغْفِرَةٌ، وَآخِرُهُ عَثَقٌ مِنَ النَّارِ، مَنْ خَفَّفَ عَنْ مَمْلُوكِهِ غَفَرَ اللَّهُ لَهُ، وَأَعْتَقَهُ مِنَ النَّارِ]

[Wakasema Maswahaba: Sio sisi sote tunapata kile cha kumfuturisha mwenyekufunga, Mtume akasema: Allah anampa thawabu hizi yule atakaemfuturisha mwenye kufunga kwa kumpa Tende, au kumnywesha Maji, au sehemu ndogo ya Maziwa yaliyochanganywa na Maji, nao ni mwezi ambao mwanzo wake ni Rehman, na katikati yake ni Msamaha, na mwisho wake ni kuacha huru na moto, atakaemfanyia wepesi mtumwa wake, Allah atamsamehe yeye, na atamuacha huru na moto]

[وَأَسْتَكْثَرُوا فِيهِ مِنْ أَرْبَعِ خِصَالٍ: خَصَلْتَيْنِ تُرْضُونَ بِهِمَا رَبَّكُمْ، وَخَصَلْتَيْنِ لَا غِنَى بِكُمْ عَنْهُمَا، فَأَمَّا الْخَصَلَتَانِ اللَّتَانِ تُرْضُونَ بِهِمَا رَبَّكُمْ، فَشَهَادَةُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَتَسْتَغْفِرُونَهُ، وَأَمَّا اللَّتَانِ لَا غِنَى بِكُمْ عَنْهُمَا، فَتَسْأَلُونَ اللَّهَ الْجَنَّةَ، وَتَعُوذُونَ بِهِ مِنَ النَّارِ، وَمَنْ أَشْبَعَ فِيهِ صَائِمًا، سَقَاهُ اللَّهُ مِنْ حَوْضِي شَرْبَةٍ لَا يَظْمَأُ حَتَّى يَدْخُلَ الْجَنَّةَ].

[Na kithirisheni ndani yake kufanya mambo manne, mambo mawili mtamridhisha kwayo Mola wenu, na mambo mawili hamjikwasii kwa kuyaacha mambo hayo. Ama mambo mawili ambayo mtamridhisha kwayo Mola weni ni: Shahada LAA ILAAHA ILLAL LAAH, na kumtaka msamaha. Ama mambo mawili ambayo hamjikwasii kwa kutokuwa nayo, mtamuomba Allah pepo, na mtajilinda kwake na moto, na atakaemshibisha ndani yake mwenye kufunga, Allah atamnyweshwa kutoka kwenye Hodhi yangu mnywesho ambao hatopata kiu mpaka aingie peponi].

Wanachuoni waliyopokea hadithi hii katika vitabu vyao

Hadithi hii imepokelewa kwa njia mbili kutoka kwa Saidi Bin Musayyab.

Njia ya kwanza: Ni hiyo niliyoitaja hapo juu, iliyopokelewa na Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan, kutoka kwa Saidi Bin Musayyab, kutoka kwa Swahaba Mtukufu Salmaan Al-faarisiy.

Na njia hii imepokelewam na:

1. Ibnu Abi Dunyaa (Kf. 281^H=894^M), katika kitabu chake: **Fadhaailu Ramadhan**, Uk. 69, Hadithi Na. 41.
2. Bin Khuzaymah (Kf. 311^H=923^M), katika kitabu chake: **Sahihu Bin Khuzaymah**, Jz. 3, Uk. 191, Hadithi Na. 1887.
3. Al-muhaamilyiy (Kf. 330^H=941^M), katika kitabu chake: **Amaalil Muhaamilyiy**, Uk. 286, Hadithi Na. 293.
4. Bin Shaahiin (Kf. 385^H=995^M), katika kitabu chake: **Fadhaailu Shahri Ramadhan**, Uk. 37, Hadithi Na. 15.
5. Al-bayhaqiy (Kf. 458^H=1066^M), katika vitabu vyake viwili
1: **Al-jaami-'u Li-shu-'abil Iman**, Jz. 5, Uk. 223, Hadithi Na. 3336.
2: **Fadhaailul Aw-qaat**, Uk. 38, Hadithi Na. 47, na 51.
6. Al-waahidiy (Kf. 468^H=1072^M), Katika tafsiri yake: **Al-waswiitw Fii Tafsiriil Qur-aanil Majiid**, Jz. 1, Uk. 277.
7. Abu Twaahir Ibnu Abi Swaq-ri (Kf. 476^H), katika kitabu chake: **Mashiikhatu Abi Twaahir**, Uk. 112, Hadithi Na. 43.
8. Al-baghawiy (Kf. 516^H), katika kitabu chake: **Tafsiiirul Baghawiy**, au kwa jina lingine: **Ma-aalimu Tanziil**, Jz. 2, Uk. 202.
9. Al-asw-bahaniy (Kf. 535^H=1141^M), katika kitabu chake: **Attar-ghiiib Wattar-hiib**, Jz. 2, Uk. 349, Hadithi Na. 1753.

10. Abduswamad Bin Asaakir (Kf. 686), katika kitabu chake: **Ahaadiithu Shahri Ramadhaan**, Uk. 36, Hadithi Na. 7.

Njia ya pili: Imepokelewa na **Abdullahi Bin Bakri Assah-miy**, ambaye kuna wakati anapokea hadithi hii kutoka kwa:

- **Iyyaas Bin Abdil Ghaffaar**, kutoka kwa **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**, kutoka kwa **Saidi Bin Musayyab**, kutoka kwa **Salmaan Al-faarisiy**

Na wakati mwingine anapokea hadithi hii hii kutoka kwa

- **Iyyaas Bin Abi Iyyaas**, kutoka kwa **Saidi Bin Musayyab**, kutoka kwa **Salmaan Al-faarisiy**, bila ya kumtaja **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**.

Na wakati mwingine anapokea hadithi hii hii kutoka kwa

- **Iyyaas Bin Abi Iyyaas**, kutoka kwa **Aliy Bin Zayd** kutoka kwa **Saidi Bin Musayyab**, kutoka kwa **Salmaan Al-faarisiy**.

Njia hii ikawa na utata kutokana na sababu mbili


- **Sababu ya kwanza:** **Iyyaas Bin Abdilghaffaar** na **Iyyaas Bin Abi Iyyaas**, je huyu **Abdulghaffaar** ndiye **Abu Iyyaas**, au hawa ni watu wawili tofauti?.

Kuna wanaoona hawa ni watu wawili tofauti, na kuna wanaoona huyu ni mtu mmoja, na wakahukumu kuwa; **Abdulghaffaar** aliyetajwa kwa jina lake, ndie huyu huyu **Abu Iyyaas** aliyetajwa kwa kunia yake, kutokana na hili wakamtia katika makosa **Abdullahi Bin Bakri** kutokana na kutatiza majina haya.

- **Sababu ya pili:** Huyu **Iyyaas Bin Abi Iyyaas**, kuna wakati anapokea Hadithi hii kutoka kwa **Saidi Bin Musayyab** moja kwa moja, na kuna wakati anapokea hadithi hii kutoka kwa **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**.

Baada ya wanachuoni wa elimu hii kulifuatilia tatizo hili na kutafuta ufumbuzi wake, wakabainikiwa kuwa: **Tatizo hili limeletwa na Abdillahi Bin Bakri**.

Hayo ndio maelezo kwa ufupi mno kuhusu hii njia ya pili, pamoja na kutaja tatizo na ufumbuzi wake, kwa faida zaidi rudi katika vitabu tulivyovitaja hapo nyuma, au angalia mchoro huu



Njia hii ya pili imepokelewa na:

1. **Al-haarith Bin Abi Usaamah** (Kf. 282^H=896^M), katika kitabu chake: **Musnadul Haarith**, au kwa jina lingine: **Bugh-yatul Baahith An Zawaaidd Musnadil Haarithi**, kilichopangiliwa na Al-haafidh Alhaythamiy (Kf. 807^H=1405^M), Jz. 1, Uk. 412, Hadithi Na. 321.
2. **Al-'uqay-liy** (Kf. 322^H=934^M), katika kitabu chake: **Kitaabu Dhu-'afaaul Kabiir**, Jz. 1, Uk. 35, Tarjama Na. 17.
3. **Ibnu Abi Haatim** (Kf. 327^H=938^M), katika kitabu chake: **Al-'ilalul Kabiir**, Jz. 5, Mjeledi wa 3, Uk. 109, Mas-ala ya 733.
4. **Abubakar Al-bayhaqiy** (Kf. 458^H=1066^M), katika kitabu chake: **Aljaami-'u Li-shu-'abil Iiman**, Jz. 5, Uk. 223, Hadithi Na. 3336.
5. **Al-khatwiibul Bagh-daadiy** (Kf. 463^H=1072^M), katika kitabu chake: **Taariikhu Madiinati Salaam**, maarufu kwa jina la: **Taariikhul Bagh-daadiy**, Jz. 5, Uk. 546, Tarjama Na. 2422.
6. **Assuyuutwiyy** (Kf. 911^H=1505^M), katika kitabu chake: **Bugh-yatul Wu-'aatu Fii Twabaqaatil Lughawiiyiina Wannuhaat**, Jz. 2, Uk. 410, Hadithi Na. 33.

Hatua ya pili Hukumu ya hadithi hii

Wanachuoni wote wa Hadithi wamekubalina kuwa hadithi hii ni **Hadithi Dhaifu tena Munkar**, na hakuna hata mmoja katika wao aliyesema kuwa hadithi hii ni **Hasan**, achilia mbali kuwa **Sahihi**.

Miongoni mwa wanachuoni hao ni:

1. **Imamu Bin Khuzayma** katika Sahihi yake, Jz. 3, Uk. 191, akaweka anawani katika Mlango wa 8, isemayo:

[بَابُ فَضَائِلِ شَهْرِ رَمَضَانَ إِنَّ صَحَّ الْخَبْرُ]

[Huu ni mlango unaoelezea fadhila za Mwezi wa Ramadhani ikiwa itasihi habari]

Aliposema:

[إِنَّ صَحَّ الْخَبْرُ]

[Ikiwa habari itasihi]

Ni dalili ya wazi kuwa; Imamu Bin Khuzaymah pamoja na kuipokea hadithi hii katika Sahihi yake, lakini ametilia kusihi kwake, kutokana na sanadi yake kupitia kwa **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**, hamtegemei kama alivyolisema Sheikh Al-baaniy katika **Sil-sila** baada ya kuitaja hadithi hii, akasema:

[وَهَذَا سَنَدٌ ضَعِيفٌ مِنْ أَجْلِ عَلِيِّ بْنِ زَيْدِ بْنِ جُدْعَانَ، فَإِنَّهُ ضَعِيفٌ كَمَا قَالَ أَحْمَدُ وَغَيْرُهُ، وَبَيَّنَّ السَّبَبَ الْإِمَامُ ابْنُ خُزَيْمَةَ فَقَالَ: "لَا أَحْتَجُّ بِهِ لِسُوءِ حِفْظِهِ". وَلِذَلِكَ لَمْ أَرَوْى هَذَا الْحَدِيثَ فِي صَحِيحِهِ قَرَنَهُ بِقَوْلِهِ: "إِنَّ صَحَّ الْخَبْرُ"]

[Na hii sanadi ni dhaifu kwaajili ya **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**, kwa sababu yeye ni dhaifu kama alivyosema Imamu Ahmad na wengineo, na amebainisha sababu Bin Khuzaymah, akasema: “Sifanyi hoja kupitia kwake kutokana na ubaya wa hifdhi yake”. Na kwaajili hiyo wakati alipoipokea hadithi hii katika Sahihi yake, akaambatanisha na kauli yake: “Ikiwa itasihi habari”]

2. Imamu Bin Abi Haatim katika kitabu chake: Al-'ilul Kabiir, aliposema kumuuliza baba yake:

[وَسَأَلْتُ أَبِي عَنْ حَدِيثِ حَدَّثَنَاهُ الْحَسَنُ بْنُ عَرَفَةَ، عَنْ عَبْدِ اللَّهِ بْنِ بَكْرِ السَّهْمِيِّ، قَالَ: حَدَّثَنَا إِيَّاسُ، عَنْ عَلِيِّ بْنِ زَيْدِ بْنِ جُدْعَانَ، عَنْ سَعِيدِ بْنِ الْمُسَيَّبِ، أَنَّ سَلْمَانَ الْفَارِسِيِّ قَالَ: خَطَبَنَا رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ آخِرَ يَوْمٍ مِنْ شَعْبَانَ.....]

[Nilimuuliza baba yangu kuhusiana na hadithi ambayo ametuhadithia sisi Hasan Bin Arafah, kutoka kwa Abidllahi Bin Bakri Assah-miy, amesema: Ametuhadithia sisi Iyyaas, kutoka kwa **Aliy Bin Zayd Bin Jud-'aan**, kutoka kwa Saidi Bin Musayyab kwamba Salmaan Al-faarisiy amesema: Alituhutubia sisi Mtume wa Allah (Swallal Lahu Alayhi Wasallam) siku ya mwisho katika Mwezi wa Shabani.....], kisha akaitaja hadithi hii kwa ufupi.

Baba yake akasema:

[هَذَا حَدِيثٌ مُنْكَرٌ]

[Hii ni Hadithi Munkar]

3. Sheikh Al-baaniy, alipoitaja hadithi hii katika vitabu vyake viwili:

1. Silsitu Ahaadiithi Dhaiifah, Jz. 2, Uk. 262, Hadithi Na. 871.
2. Dhaiifu Tar-ghiiib Wattar-hiib, Jz. 1, Uk. 296, Hadithi Na. 589.

Akasema **Hadithi hii ni Munkar**

Hawa ni wanachuoni watatu katika jumla ya wanachuoni wengi waliyoikataa hadithi hii, na wote wakatoa hukumu moja.

Faida muhimu

Faida ya kwanza: Kuna baadhi ya Masheikh katika zama zetu walijaribu kuitetea na kuipa nguvu hadithi hii, wakafikia hatua ya kuandika risala maalumu katika jambo hilo lakini hawakupatia katika jitihada zao, kutokana na kwenda kinyume na kauli za wanachuoni wenye kutegemewa katika jambo hili wa zamani na wa sasa.

Miongoni mwa Masheikh hao ni **Sheikh Abu Abdirahmani Bin Aqil Adhwaahiriy**, katika risala yake aliyoiita:

[الْبُرْهَانُ عَلَى تَحْسِينِ حَدِيثِ سَلْمَانَ]

[Al-bur-haan Alaa Tahsiin Hadiith Sal-maan]

Akajibiwa na **Sheikh Aliy Bin Hasan Al-halabiy** kwenye risala yake aliyoiita:

[تَنْقِيحُ الْأَنْظَارِ بِضَعْفِ حَدِيثِ: رَمَضَانَ أَوَّلُهُ رَحْمَةٌ، وَأَوْسَطُهُ مَغْفِرَةٌ، وَآخِرُهُ عِتْقٌ مِنَ النَّارِ]

[Tanqiihul Andhwaar Bidhwa-'afi Hadiith Ramadhaan Awwaluhuu Rahmah, Wa-aw-satwuhuu Magh-firah, Wa-aakhiruhuu It-qun Mina Naar].

Fadia ya pili: Kuna baadhi ya Masheikh na waandishi wamejitahidi kukusanya hadithi dhaifu zinazohusiana na fungu, na nimefanikiwa kuona risala ya mmoja wao ambae ni Sheikh Ahmad Bin Abdillahi Assulamiy, na risala yake akaiita:

[خَمْسُمِائَةِ حَدِيثٍ لَمْ تَثْبُتْ فِي الصِّيَامِ، وَالِإِعْتِكَافِ، وَزَكَاةِ الْفِطْرِ، وَالْعِيدَيْنِ، وَالْأَضَاحِي]

[Khamsumiati Hadiithin Lam That-but Fisswiyaami, Wali-'itikaaf, Wazakaatil Ftw-ri, Wal-'iidayni, Wal-adhwaahiy].

Baada ya maelezo haya, nakuomba ewe muislamu na mwanafunzi mwenzangu ufahamu kuwa hadithi hii haikuthibiti kwa Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) hivyo ukimsikia mtu yoyote anaitaja hadithi hii, basi mkumbushe na mjulishe ujumbe huu.

Kwa nini Hadithi hii ikawa ni Munkar?.

Kabla sijajibu swali hili, ni muhimu kufahamu kuwa Hadithi Munkari ni katika jumla ya Hadithi Dhaifu, na Hadithi Dhaifu ni:

[مَا لَمْ يَجْمَعْ صِفَةَ الصَّحِيحِ أَوْ الْحَسَنِ]

[Ile Hadithi ambayo haijakusanya sifa za Hadithi Sahihi au Hadithi Hasan]

⇒ Tazama kitabu: Attaq-riib, cha Imamu Nawawiy, Uk: 31

Na sifa za Hadithi Sahihi ni:

[اتَّصَالَ السَّنَدِ بِنَقْلِ الْعَدْلِ تَامَ الضَّبْطِ عَنْ مِثْلِهِ إِلَى مُنْتَهَاهُ وَلَا يَكُونُ شَاذًا وَلَا مُعَلَّلًا]

[Ni kuungana sanadi yake kwa kunukuliwa na mpokezi muadilifu ambaye hifdhi yake imetimia, kutoka kwa mpokezi mfano wake mpaka mwisho wa hadithi hiyo, na isiwe shadhi wala na kasoro].

⇒ Tazama:

1. Qaamuus Mustwalahaatil Hadiith, cha Muhammad Swidiq Minshawiy, Uk. 72.
2. Mu-'ujam Mustwalahaatil Hadiith, cha Sulayman Musallam na mwenzake, Uk. 70.

Ama sifa ya Hadithi Hasan ni:

[اتَّصَالَ السَّنَدِ بِنَقْلِ الْعَدْلِ خَفِيفِ الضَّبْطِ عَنْ مِثْلِهِ إِلَى مُنْتَهَاهُ وَلَا يَكُونُ شَاذًا وَلَا مُعَلَّلًا]

[Ni kuungana sanadi yake kwa kunukuliwa na mpokezi muadilifu ambaye hifdhi yake imepungua kidogo, kutoka kwa mpokezi mfano wake mpaka mwisho wa hadithi hiyo, na isiwe shadhi wala na kasoro].

Tofauti ya sifa kati ya Hadithi Sahihi na Hadithi Hasan, ni Hifdhi ya mpokezi. Katika Hadithi Sahihi, hifdhi ya mpokezi inatakiwa iwe imetimia na kuwa

katika kiwango cha juu, ama katika **Hadithi Hasan**, hifdhi ya mpokezi inatakiwa iwe imepungua kidogo, na iwe chini ya kiwango cha mpokezi wa **Hadithi Sahihi**.

Ukikusanya sifa za za **Hadithi Sahihi** na **Hadithi Hasan**, utaona zinadhibitika katika sehemu kuu tano, nazo ni:

1. Kuungana kwa sanadi
2. Uadilifu wa wapokezi
3. Udhibiti (uwezo wa kuhifadhi) wa wapokezi wake
4. Kukosekana Ushudhuudh
5. Kukosekana kasoro

Ufafanuzi wa kila sifa moja miongoni mwa sifa hizi, na namna ya kupatikana kwake na kuithibitisha kwa mpokezi na kila hadithi, utaupata katika vitabu vya **Elimu ya Mustwalahul Hadiith**.

Ikiwa itakosekana sifa moja miongoni mwa sifa hizi katika hadithi yoyote ile, basi hadithi hiyo inakuwa ni **Dhaifu**, na kila sifa hizi zinapozidi kupungua katika hadithi, ndivyo hadithi nayo inavyozidi kuwa **Dhaifu zaidi**.

Baada ya maelezo haya kwa ufupi kuhusu **Hadithi Dhaifu**, sasa turudi katika nukta yetu ya kujua **Hadithi Munkar**.

Hadithi Munkar, ni:

[مَا رَوَاهُ الضَّعِيفُ مُخَالَفًا لِمَا رَوَاهُ الثَّقَاتُ]

[Hadithi ambayo ameipokea mpokezi dhaifu hali ya kuwa ni mwenye kukhalifiana na hadithi ambayo ameipokea mpokezi muadilifu]

⇒ Tazama:

1. Qaamuus Mustwalahaatil Hadiith, Uk. 135.
2. Mu-'ujam Mustwalahaatil Hadiith, Uk. 123.

Tumeona katika sifa za **Hadithi Sahihi** na **Hadithi Hasan**, ni mpokezi wa hadithi hizo awe muadilifu, na kinyume cha muadilifu ni dhaifu, udhaifu huo unaweza kuwa ni mkubwa au mdogo kulingana na hali ya mpokezi wa hadithi husika.

Mpokezi anapokuwa dhaifu, sifa hii inapelekea hadithi zake zikataliwe, na ikitokea hadithi yake imetofautiana na hadithi ya muadilifu, basi udhaifu wake unazidi mara mbili, na hapo hadithi yake itaitwa **Munkar**.

Kwa mfano:

Tuna wapokezi wawili wa hadithi

1. **Muhammad Bin Ismaili** na
2. **Abdillahi Bin Sabai**

Muhammad Bin Ismaili akasimulia Hadithi isemayo: **Maswahaba wote wa Mtume ni watu wema, na wote wataingia peponi, bila ya kuzingatia kuwahi kusilimu kwao au kuchelewa, kusuhubiana na Mtume kwa muda mrefu au mfupi.**

Abdillahi Bin Sabai nae akasimulia hadithi isemayo: **Baadhi ya Maswahaba wa Mtume ni watu wema, na wengine ni waovu, wema ndio wataingia peponi, na waovu wataingia motoni.**

Hizi ni hadithi mbili zinazowazungumzia watu wa aina moja, nao ni Maswahaba, na wasimulizi wa hadithi hizi wametafautiana, tofauti ambayo hatuwezi kuzikusanya tukapata kitu kimoja, kwani mmoja anathibitisha wema kwa Maswahaba wote, na mwingine akawagawa Maswahaba katika makundi mawili, wema na waovu.

Ikitokea hali kama hii katika hadithi yoyote, basi wanachuoni wa hadithi huchukua hatua kadhaa ili kutafuta ufumbuzi, miongoni mwa hatua hizo ni kufuatilia hali za wapokezi wa hadithi hizo.

Wakikuta mpokezi mmoja ni muadilifu na mwingine ni dhaifu, basi wanaichukua hadithi ya mpokezi muadilifu, na kuiacha hadithi ya mpokezi dhaifu, na hii hadithi ya mpokezi dhaifu ndio inaitwa **Munkar**, na ya mpokezi muadilifu inaitwa **Maaruuf**.

Kama katika huu mfano wetu, tulipowachunguza hawa wapokezi wawili, tukamkuta **Muhammad Bin Ismaili** ni mtu muadilifu, na **Abdillahi Bin Sabai** ni mtu dhaifu, hivyo katika hali hii, ile hadithi ya Muhammad Bin Ismaili itaitwa **Maaruuf** na ndiyo itakayofanyiwa kazi, na hii ya Abdillahi Bin Sabai itaitwa **Munkar**, nayo haitofanyiwa kazi.

Hadithi ya makumi matatu

Baada ya kutoa maelezo kwa ufupi kuhusiana na **Hadithi Sahihi, Hasan, Dhaifu** na kumaliza na **Hadithi Munkar** ambayo ni katika jumla ya **Hadithi Dhaifu**, sasa hebu tujue japo kwa ufupi sababu iliyopelekea hadithi hii kuwa ni **Munkar**.

Wameeleza wanachuoni sababu nyingi, ila mimi nitataja sababu mbili kwaajili ya kufupisha.

Sababu ya Kwanza:

Ni kutokana na riwaya zote za hadithi hii kupitia kwa wapokezi dhaifu ambao ni:

1. **Aliy Bi Zayd Bin Jud-'aan**
2. **Iyyaas Bin Abi Iyyaas**
3. **Iyyaas Bin Abdilghaffaar**

Ikiwa tutahukumu hawa ni watu wawili tofauti, basi wote ni madhaifu, na ikiwa tutahukumu kuwa ni mpokezi mmoja isipokuwa majina yao ndio yalititiza, pia ni madhaifu.

Sababu ya pili:

Ni kupatikana baadhi ya vipengele katika hadithi hii vinapingana na **Hadithi Sahihi**, kama kipengele alichosema:

[وَهُوَ شَهْرٌ أَوَّلُهُ رَحْمَةٌ، وَأَوْسَطُهُ مَغْفِرَةٌ، وَآخِرُهُ عَذَابٌ مِنَ النَّارِ]

[Nao ni mwezi ambao mwanzo wake ni Rehma, na katikati yake ni Msamaha, na mwisho wake ni Kuachwa Huru na Moto] Kipengele ambacho ndio kilichobeba maudhui ya risala hii.

Ufafanuzi wa sababu hizi

Ama kuhusiana na sababu ya kwanza, nayo ni udhaifu wa wapokezi ukirejea vitabu vitatu nilivyovitaja katika Uk, utapata kauli hizo, pia ukirudi katika vitabu vilivyotaja hadithi hizo, wahakiki wa vitabu hivyo wamebaini hali za wapokezi hawa.

Ama sababu ya pili, nayo ni kupatikana vipengele kadhaa katika hadithi hii vimekhalifiana na Hadithi Sahihi, hasa kipengele cha **Makumi Matatu ya Ramadhani**, ufafanuzi wake kwa ufupi ni kama ifuatavyo.

Kumi la Rehma na Kuachwa Huru na Moto

Kipengele hiki kinakinzana na Hadithi nyingi Sahihi, miongoni mwa hadithi hizo ni hadithi ya Abu Hurayra, iliyotajwa na Imamu Tirmidhiy katika Sunani yake, amesema Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam):

[إِذَا كَانَ أَوَّلُ لَيْلَةٍ مِنْ شَهْرِ رَمَضَانَ، صَقَدَتِ الشَّيَاطِينُ، وَمَرَدَةُ الْجِنِّ، وَغَلِقَتْ أَبْوَابُ النَّارِ، فَلَمْ يُفْتَحْ مِنْهَا بَابٌ، وَفُتِحَتْ أَبْوَابُ الْجَنَّةِ، فَلَمْ يُغْلَقْ مِنْهَا بَابٌ، وَيُنَادِي مُنَادٍ: يَا بَاغِيَ الْخَيْرِ أَقْبِلْ، وَيَا بَاغِيَ الشَّرِّ أَقْصِرْ، وَلِلَّهِ عِتْقَاءُ مِنَ النَّارِ، وَذَلِكَ كُلُّ لَيْلَةٍ].

[Unapokuwa usiku wa kwanza katika mwezi wa Ramadhani, huzuiliwa Mashetani, na Majini waovu, na hufungwa milango ya moto, na haufunguliwi mlango wowote katika milango hiyo. Hufunguliwa milango ya pepo, na haufungwi mlango wowote katika milango hiyo, na ananadi mwenye kunadi: Ewe mwenye kutafuta kheri, elekea kwenye kheri, na ewe mwenye kutafuta shari punguza kufanya shari, na Allah huacha huru watu na moto, na hilo ni katika kila usiku].

⇒ Tazama: Sunanu Tirmidhiy, Hadithi Na. 682

Hadithi Sahihi inasema:

- Allah anafungua milango ya pepo, na kufunga milango ya moto, anawazuwia mashetani, na hii ndio rehma kubwa kwa waja ndani ya mwezi huu, na huanza tu Ramadhani inapoingia.

Hadithi Munkar inasema:

- Allah hufungua rehma zake kumi la kwanza tu.

Hadithi Sahihi inasema:

- Kila usiku mmoja Allah huacha huru watu na moto.

Hadithi Munkari inasema:

- Ikifika kumi la mwisho Allah ndio huacha huru watu na moto.

Kumi la Msamaha

Hadithi Munkari inasema:

- Kumi la pili ndio Kumi la Msamaha

Hadithi Sahihi inasema:

- Msamaha upo kwa kila anayefunga Ramadhani.

Amesimulia Abu Hurayra kuwa Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) amesema:

[مَنْ صَامَ رَمَضَانَ، إِيمَانًا وَاحْتِسَابًا، غُفِرَ لَهُ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِهِ]

[Atakaefunga Ramadhani hali ya kuwa ana imani na kutarajia malipo kwa Allah, atasamehewa madhambi yaliyotangulia]

⇒ Tazama: Sahihul Bukhari, Hadithi Na. 38

Huu ni uchambuzi mdogo sana unaohusu kipengele kimoja katika Hadithi ya Makumi Matatu na namna inavyotofautiana na Hadithi Sahihi.

Katika **Hadithi ya Makumi Matatu**, vipo vipengele vingi sana vimetofautiana na Hadithi nyingi Sahihi, lau si kuhofia kurefusha makal hii basi ningekubainishia kila kipengele, lakini makamu hainiruhusu.

Kwakuwa kipengele hiki ni maarufu kwa wasmeji wengi wa dini, basi nimeona nitosheka nacho.

HITIMISHO

Katika kuhitimisha makala hii, napenda kumshukuru Allah (Jalla Waalaa) kwa mara nyingine, kwa kunijaalia kumaliza amali hii tukufu ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Napenda kutoa wito kwa waislamu wote kuwa, tujihadhari sana kutumia Hadithi Dhaifu na za Uongo katika jambo lolote la dini, kwani jambo hili limekatazwa, na Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam) amemsema vibaya mwenye kumzulua uongo.

Wanachuoni wa Hadithi (Allah awarehemu) wametoa juhudi kubwa katika kuzilinda Hadithi za Mtume (Swallal Laahu Alayhi Wasallam), ili kuenzi juhudi hizo, ni vizuri sisi waislamu tujitahidi sana kutumia vitabu vyao katika kujua Hadithi Sahihi na kuzifanyia kazi, pia kujua Hadithi Dhaifu na kujitenga na kujitenga nazo.

Hadithi ya **Makumi Matutu ni Hadithi Munkari** kutokana na kupokelewa na wapokezi dhaifu, pia kutofautiana na Hadithi Sahihi, hivyo natumai ewe ndugu msomaji utakuwa umeelewa maudhui hii kwa uzuri

Tunamwomba Allah atujaalie tuwe ni katika wale wenye kusikia na kufuata yaliyomema, atujaalie tuwe ni katika wale wenye kutumia **Hadithi Sahihi** na kuachana na **Hadithi Dhaifu**.

وصلى الله على محمد وعلى آله وصحبه وسلم

وأخردعائي

﴿إِنَّ الْحَمْدَ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ﴾

[يونس: ١٠]

Abu Anas

Ismaili Bin Musa Bin Kiza

Markaz Bin Taymiyyah

Pongwe – Tanga – Tanzania

Al-khmisi, 7-Ramadhani-1440^H = 30-April-2020^M

Tel: 0713 006 669 – 0756 663 344

0693 342 827 – 0734 129 012

VITABU MAREJEO

- 1. Ahaadiithu Shahri Ramadhaan**
Abul Yumni, Abduswamad Bin Asaakir (Kf. 686), Mhakiki: Aliy Bin Hasan Bin Aliy Bin Abdilhamid Al-athariy, Chp. 1, Mwk. 1418^H=1998^M, Daru Affaan, Saudi Arabia.
- 2. Al-jaami-'u Li-akhlaaqi Raawiy Wa-aadaabi Saami-'ii**
Abu Bakri, Ahmad Bin Aliy Bin Thabit Al-khatwiibul Bagh-daadiy (Kf.463^H=1072^M), Mhakiki: Abu Abdirahmani Swalaahu Bin Muhammad Bin Uway-dhwa, Chp. 1, Mwk. 1417^H=1996^M, Darul Kutub Il-miyah, Beirut - Lebanon.
- 3. Al-jaami-'u Li-shu-'abil Iimaan**
Abu Bakri Ahmad Bin Husein Al-bayhaqiy (Kf.458^H=1066^M), Chp. 1, Mwk. 1423^H=2003^M, Maktabatu Rushd, Riyadh - Saudi Arabia.
- 4. Al-la-aalul Masw-nuu-'ah Fil Ahaadiithil Maw-dhwuu-'ah**
Jalaalu Diin Abdurahman Bin Abibakri Assuyuutwiyy (Kf. 911^H=1505^M), Chp ya Darul Ma-'arifah, Beirut - Lebanon.
- 5. Al-Mugh-niy Fii Dhwu-'afaai**
Shamsu Diin, Abu Abdillahi, Muhammad Bin Ahmad Bin Othman Addhahabiy (Kf.748^H= 1347^M), Mhakiki: Nuur Diin Itr, Dar Ih-yaa'i Turaath, Qatar
- 6. Al-musnad**
Imamu Ahmadi Bin Muhammad Bin Hanbal (Kf. 241^H=855^M), Mhakiki: Shuaybul Ar-naauutw na wenzake, Chp. 1, Mwk. 1420^H=1999^M, Muassasatu Risaalah, Beirut - Lebanon.
- 7. Al-waswiitw Fii Tafsiiril Qur-aanil Majiid.**
Abul Husein Aliy Bin Ahmda Al-waahidiy (Kf. 468^H=1072^M), Mhakiki: Aadil Ahmad Abdulmawjud na wenzake, Chp. 1, Mwk. 1415^H=1994^M, Darul Kutub Ilmiyyah, Beirut - Lebanon.
- 8. Amaalil Muhaamiliy**
Husein Bin Ismaili Bin Muhamma Al-muhaamiliy (Kf. 330^H=941^M), Mhakiki: Dkt. Ibrahim Bin Ibrahim Al-qaysiy, Chp. 1, Mwk. 1412^H=1991^H, Maktabatul Islaamiy, Oman - Jordan, na Daru Ibnul Qayyim, Dammaam - Saudi Arabia
- 9. Attaq-riib Wattaysiir Lima-'arifati Sunanil Bashiir Nadhiir**
Muhyidiin Sharafu Nawawiy (Kf. 676^H=1278^M), Mhakiki: Muhammad Othman Alkhast, Chp. 1, Mwk. 1405^H=1985^M, Darul Kitaab Al-'arabiy, Beirut - Lebanon.
- 10. Attar-ghiib Wattar-hiib**
Abul Qasim Ismail Bin Muhammad Ibnul Fadhl Al-asw-bahaniy (Kf. 535^H=1141^M), Mhakiki: Ayman Bin Swaleh Bin Shaban, Chp. 1, Mwk. 1414^H=1993^M, Darul Hadith, Cairo - Misr.
- 11. Bugh-yatul Wu-'aatu Fii Twabaqaatil Lughawiyyiina Wannuhaat**
Jalaalu Diin Abdurahman Bin Abibakri Assuyuutwiyy (Kf. 911^H=1505^M), Mhakik: Muhammad Abul Fadhl Ibrahim, chapa ya Mwk. 1384^H=1965^M.
- 12. Fadhaailu Ramadhan**
Abu Bakri Abdullahi Bin Muhammad Bin Abi Dunyaa (Kf.281^H=894^M), Mhakiki: Abdullahi Bin Hamad Al-mansour, Chp. 1, Mwk. 1415^H=1995^M, Daru Salaf, Riyadh - Saudi Arabia.
- 13. Fadhaailu Shahri Ramadhaan**
Abu Hafs, Omar Bin Ahmad Bin Shaahiin (Kf.385^H=995^M), Mhakiki: Samir Bin Amin Azzuhayriy, Chp. 2, Mwk. 1410^H=1990^M, Maktabatul Manaar, Zar-qaa - Jordan
- 14. Fadhaailul Aw-qaat**
Abu Bakri Ahmad Bin Husein Al-bayhaqiy (Kf.458), Mhakiki: Khilaaf Mahmoud Abdusamii, Chp. 1, Mwk. 1417^H=1997^M, Darul Kutub Ilmiyyah, Beirut - Lebanon.

15. **Khamsumiati Hadiithin Lam That-but Fisswiyaami, Wali-'itikaaf, Wazakaatil Ftw-ri, Wal-'iidayni, Wal-adhwaahiy**
Sheikh Ahmad Bin Abdillahi Assulamiy, Chp. 1, Mwk. 1423H=2002M.
16. **Kitaabu Dhwu-'afaaul Kabiir**
Abu Ja-'afar Muhammad Bin Amri Bin Musa Bin Hammaad Al-'uqayliy (Kf.322^H=934^M), Mhakiki: Hamdiy Bin Abdilmajid Assalafiy, Chp. 1, Mwk. 1420^H=2000^M, Daru Swamii-'iy, Riyadh – Saudi Arabia.
17. **Kitaabul Ilalul**
Abu Muhammad Abdurahman Bin Abi Hatim (Kf. 327^H=938^M), Mhakiki: Kundi la watafiti, Chp. 1, Mwk. 1427H=206M, Riyadh – Saudi Arabia
18. **Kitaabul Maj-ruuhiin Minal Muhaddithiina**
Abu Hatim Muhammad Bin Hibbaan Al-busty (Kf. 354^H=965^M), Mhakiki: Hamdiy Bin Abdilmajid Assalafiy, Chp. 1, Mwk. 1420^H=2000^M, Daru Swamii-'iy, Riyadh – Saudi Arabia.
19. **Kitaabul Maw-dhwuu-'aatul**
Jamaalu Diin Abul Faraj Abdurahman Bin Aliy Ibnul Jawziy (Kf. 597^H=1201^M), Mhakiki: Abdurahman Muhammad Othman, Chp. 1, Mwk. 1386^H=1966^M, Maktabatu Salafiyyah, Madina – Saudi Arabia.
20. **Mashiikhatu Abi Twaahir Ibn Abi Swaq-r**
Muhammad Bin Ahmad Bin Muhammad Ibnu Abi Swaq-ri (Kf. 476^H), Mhakiki: Sharif Hatim Bin Arif Al-'awniy, Chp. 1, Mwk. 1418^H=1997^M, Maktabatu Rushd, Riyadh – Saudi Arabia.
21. **Mu-'ujam Mustwalahaatil Hadiith**
Sulayman Musallam na Husein Ismaili, Chp. 1, Mwk. 1417H=1996M, Maktabatul Abiikaan, Riyadh – Saudi Arabia.
22. **Musnadul Haarith (Bugh-yatul Baahith An Zawaaiddi Musnadil Haarithi)**
Al-haarith Bin Abi Usaamah (Kf. 282^H=896^M), Mpangaji: Al-haafidh Alhaythamiy (Kf. 807^H=1405^M), Mhakiki: Dkt. Husein Ahmad Swaleh Al-baakiriy, Chp. 1, Mwk. 1413H=1992M, Saudi Arabia.
23. **Qaamuus Mustwalahaatil Hadiith**
Muhammad Swidiq Minshawiy, Darul Fadhiilah, Cairo – Misr.
24. **Sahihu Bin Khuzaymah**
Abu Bakri Muhammad Bin Is-haq **Bin Khuzaymah** (Kf.311^H=923^M), Mhakiki: Dkt. Muhammad Mustapha Al-a-'adhwamiy, Chapa ya Mwk. 1400^H=1980^M, Maktabatul Islaamiy, Beirut – Lebanon.
25. **Sahihul Bukhari**
Muhammad Bin Ismail Al-bukhariy (Kf. 254^H=870^M), Chp. 1, Mwk. 1423^H=2002^M, Dar Bin Kathir, Dimashq.
26. **Sil-silatul Ahaadiithi Dhwa-'iifah Wal-maw-dhwuu-'ah**
Abu Abdirahman Muhammad Bin Nuuh Bin Haaj Naaswiru Diin Al-baniy (Kf.1420^H=1999^M), Chp. 1, Mwk. 1412H=1992M, Maktabatul Ma-'aarif, Riyadh – Saudi Arabia.
27. **Sunanu Abi Daud**
Abu Daud, Sulaymaan Bin Ash-'ath Al-az-diy Assijis-taaniy, (Kf. 275^H=889^M), Mhakiki: Shuaybu Ar-naauutw na Muhammad Kaamil, Chapa ya Mwk: 1430^H=2009^M, Daru Risaala Al-'aalamiyah, Dimashq – Siriya.
28. **Sunanu Tirmidhiy**
Abu Isa Muhammad Bin Isa Attirmidhiy (Kf.279H=892M), Mhakiki: Dkt. Bashar Awaad Maaruf, Chp. Mwk. 1996^M, Darul Gharbil Islaamiy, Beirut – Lebanon.

29. Taariikhu Madiinati Salaam, (Taariikhul Bagh-daadiy).

Abu Bakri, Ahmad Bin Aliy Bin Thabit Al-khatwiibul Bagh-daadiy (Kf.463^H=1072^M), Mhakiki: Dkt. Bashar Awwaad Ma-'aruuf, Chp. 1, Mwk. 1422^H=2001^M, Darul Gharbil Islaamiy, Beirut – Lebanon.

30. Tad-wiinu Sunnatin Nabawiyyah

Dkt. Muhammad Bin Matwar Azzahraaniy, Chp. 1, Mwk. 1417^H=1996^M, Darul Hijra, Rayadh – Saudi Arabia.

31. Tafsiirul Baghawiy (Ma-aalimu Tanziiil)

Abu Muhammad Husein Bin Masoud Al-baghawiy (Kf. 516^H), Mhakiki: Muhammad Abdullahi Annamr na wenzake, chapa ya Mwk. 1409^H, Daru Twayba, Riyadh – Saudi Arabia

32. Tanqiihul Andhwaar Bidhwa-'afi Hadiith Ramadhaan Awwaluhuu Rahmah, Wa-aw-satwuhuu Magh-firah, Wa-aakhiruhuu It-qun Mina Naar

Aliy Bin Hasan Bin Aliy Bin Abdilhamid Al-athariy, Chp. 1, Mwk. 1418^H=1998^M, Darul Masiir, Riyadh – Saudi Arabia

KAZI ZILIZOTOKA

1. UHARAMU WA NDOA YA MUT-'A. (SEHEMU YA KWANZA)
2. UHARAMU WA NDOA YA MUT-'A. (SEHEMU YA PILI)
3. SHIA NA MASWAHABA. (SHUBHA NA MAJIBU YAKE)

٤. رسالة في الوضوء والغسل والصلاة، للشيخ ابن عثيمين رحمه الله

5. UBAINIFU JUU YA UDHAIFU WA HADITHI YA MAKUMI MATATU YA RAMADHANI (NDIO HII IPO MIKONONI MWAKO)